


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO



*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na.CDC/05/3/VOL.III/9

06 Desemba 2020

**YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MTENDAJI WA KIJJI  
DARAJA LA III**

Kufuatia Halmashauri ya Wilaya ya Chato kupata kibali cha ajira mbadala chenye Kumb.Na.FA 170/521/01/ "b"/21 ya tarehe 11 Desemba, 2020 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu ajira Mbadala, MKurugenzi Mtendaji Wilaya ya Chato anatangaza nafasi za kazi na anakaribisha maombi kwa Watanzania wenye sifa za kujaza nafasi kama zilivyoorodheshwa katika tangazo hili:-

**MASHARTI YA JUMLA**

- I. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
- II. **Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.**
- III. Waombaji ambao tayari walishaajiriwa serikalini na wakapata Chekinamba wanashauriwa kuzingatia utaratibu wa Uhamisho au kurejea katika Utumishi wa Umma baada ya kuacha kazi kama ilivyobainishwa kwenye waraka Na ccb.228/271/01 wa tarehe 7 A gost,2012
- IV. Nafasi ya kazi inayoombwa iandikwe juu ya bahasha, kutozingatiwa hili kutasababisha maombi ya kazi kuwa batili.
- V. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- VI. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo kwa kuzingatia sifa za kazi husika. Viambatanisho hivyo vibanwe sawa sawa kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea. Picha moja (Passport size) ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- VII. Testimonials", "**Provisional Results**", "**Statement of results**", hati za matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) **HAVITAKUBALIWA.**

- VIII. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU na NECTA).
- IX. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- X. **Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua kali za kisheria.**
- XI. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni **tarehe 27 Januari, 2021**
- XII. Maombi yanaweza kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili au Kiingereza na yatumwe kupitia posta kwa anuani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHATO  
SLP.116  
CHATO -GEITA**

#### **1. MTENDAJI WA VIJJI DARAJA LA III – NAFASI NNE (4)**

##### **MAJUKUMU YA KAZI**

- Afisa masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao,kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Mendeleo ya kijiji.
- Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya kijiji
- Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa,umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika kijiji
- Kusimamia,kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.
- Mwenyekiti wa kikao cha wataalaamu waliopo katika kijiji
- Kupokea kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji na
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

##### **SIFA ZA MWOMBAJI**

- Kuajiriwa mwenye elimu ya Kidato cha nne/sita aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti Katika moja wapo ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma, Chuo cha Maendeleo Mipango na Maendeleo Vijijini (Mipango) au chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

## MSHAHARA

- Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali yaani **TGS B1** kwa mwezi.

Imetolewa na;



E.L. Mwaiteleke  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**CHATO**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
S. L. P. 116  
CHATO